

MUNGU ANAYE

MWANA-KONDOO ALIYETOLEWA



Hebu na tusome kutoka kwenye—kwenye Kitabu cha Marko Mtakatifu, ninaamini ningesoma, nimechagua kusoma kidogo na kupazungumzia, na kifungu cha 46 cha ninii—cha mlango wa 10. Na tusimame kwa heshima ya Neno, wakati tunaposoma. Neno ni Mungu. Sote tunajua hilo. Kwa hiyo simameni, mwonyeshe utii, jambo ambalo mnapaswa kufanya; ninyi husimama kuipigia saluti bendera ikipitishwa; mbona si Neno la Mungu wakati linaposomwa?

Wakafika Yeriko; hata walipokuwa wakishika njia kutoka Yeriko, pamoja na wanafunzi wake, na mkutano mkubwa, mwana wa Timayo, Bartimayo, yule muombaji kipofu, alikuwa ameketi kando ya njia.

Naye aliposikia ya kwamba ni Yesu Mnazareti, alianza kupaza sauti yake, na kusema, Mwana wa Daudi, Yesu, unirehemu.

Na wengi wakamkemea ili anyamaze, lakini alizidi kupaza sauti, Mwana wa Daudi, unirehemu.

Yesu akasimama, akasema, Mwiteni. Wakamwita yule kipofu, wakamwambia, Jipe moyo, inuka, anakuita.

Akatupa vazi lake, akaruka, akamwendea Yesu.

Yesu akamjibu, akamwambia, Wataka nikufanyie nini? Yule kipofu akamwambia, Bwana wangu, nataka nipate kuona.

...Yesu akamwambia, Enenda zako, imani yako imekuponya. Mara akapata kuona; akamfuata Yesu njiani.

² Na tuombe. Roho Mtakatifu Mkuu, lihuishe Neno hili kwetu, usiku wa leo, katika mchezo huu mdogo wa kuigiza. Jalia tuone onyesho hili likitokea tena, na, kwa kufanya hivyo, tuchukue imani kwamba Mungu angali hai, Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu, Mwanawe mpendwa, Mwokozi wetu. Amina.

Mwaweza kuketi.

³ Somo letu usiku wa leo ni: *Mungu Anaye Mwana-Kondoo Aliyetolewa.*

⁴ Na sasa asubuhi ya leo tulikuwa na wakati mzuri sana, wakati tulipomwona Yesu akiingia Yeriko. Nasi tulikuta kwamba kulikuwa na jamaa mdogo pale jina lake Zakayo, a—

alipanda juu ya mkuyu na kujificha, kwa sababu hakuamini ya kwamba Yesu alikuwa ni nabii. Lakini mke wake alikuwa ni mwanafunzi wa Yesu, naye alikuwa akimwomba. Na wakati Yesu alipokuja moja kwa moja chini ya ule mti, Yeye alisimama, akatazama juu na kumwita kwa jina lake, na kusema, “Shuka chini, ninaenda pamoja nawe nyumbani leo.” Nami nilifikiri lingekuwa ni jambo zuri usiku wa leo, pia, wakati tukiwa hapa, kwamba tungeendelea tu na Yesu. Tulimwomba asubuhi ya leo aende pamoja nasi, nasi tulitaka kwenda pamoja na Yeye, na hebu tuendeleeni tu pamoja Naye kupitia Yeriko.

⁵ Sasa, usiku wa leo, onyesho letu linafunguliwa mahali pale pale, huko Yeriko tena, Naye Yesu yumo nyumbani mwa Zakayo sasa, akila chakula Cha—Chake. Na ni siku yenye baridi ya Oktoba, na kungali ni mapema sana asubuhi, bado, nao upepo unavuma ukishuka kutoka m—mlimani. Huko juu katika Uyahudi, inakuwa baridi sana kule juu, mapema asubuhi, hasa kwenye wakati huo wa mwaka.

⁶ Nayo nchi wakati huo, kama vile ilivyo kwenye nchi hiyo ya kale sasa, imejaa ombaomba. Wanaenda kwenye kona za barabara na kuombaomba. Mimi... Huko chini kwenye nchi hizo bado, mitaa imejaa ombaomba. India na, loo, Afrika, na mahali pengi, wangali wana ombaomba; viwete, walemavu, vipofu, waliopooza. Na wakati mwingine watu wasioweza kujipatia riziki, wao wenyewe, wanaomba tu, nao wanaketi pale wakati mwingine na wanashinda na njaa.

⁷ Mimi, huko India, nimeshashuka mitaani, nikiwa na fedha ambazo nilikuwa nimepewa na watu hawa, nami nikazibadilisha kutoka kwenye dola zikawa rupii. Na kujaribu ku—kuzisambaza, mbona, iliwabidi kuleta jeshi la mgambo kuniondoa mtaani; walikuwa wakinikanyaga. Na palikuwapo na maskini wanawake wadogo wamelala pale, wakifa kwa njaa. Maskini mtoto mchanga, naye alikuwa ameshikwa na njaa sana hata nyama zilikuwa zimeshikamana na mifupa, na hata unaona mahali fuvu la kichwa lilipounganishwa. Naye anakukabidhi mtoto huyo, akijaribu kukufanya umchukue mtoto huyo asiye akafa. Ukimchukua *huyu*, vipi kuhusu *yule*, vipi kuhusu *huyu*, vipi kuhusu...? Loo, jamani, ni, una—unaninii... Kama ungeona kile tunachookota kutoka kwenye pipa la takataka hapa, karibu, kingeweza kuwalisha hao watu. Kamwe hamtambui jinsi nchi hii ilivyo tajiri, wakati unapouona ulimwengu huo mwingine ukifa kwa njaa.

⁸ Nao umejaa ombaomba. Na siku hii, wakati onyesho letu linapoanza, kulikuwako na... Tunaona ya kwamba ombaomba hawa wote walishukia, kwa kawaida, huko Yeriko, kwenye lango la kaskazini, walioshuka kutoka Yerusalemu. Yeriko haukuwa ni mji ulio tajiri sana. Lakini Yerusalemu, mahali pale pakuu penye mbwembwe, mahali maarufu pa hekalu, na—na matajiri wote walihamia Yerusalemu, nao ulikuwa ni mji mkuu wenye

madoido. Nao watu waliotoka huko kidogo walikuwa ni wenye mali. Nao wafanya biashara, na kadhalika, wakati wangeingia, mchana, ombaomba hawa walikuwa na mabanda yao; ni sheria isiyoandikwa, walijua mahali ambapo kila mmoja angekaa kwa ajili ya ninii yake, kuomba riziki yake, sadaka zake.

⁹ Nao iliwabidi kufika pale mapema wakati wafanyabiashara wanapoingia, kwa maana mtu labda alimsaidia ombaomba mmoja tu kwa siku, alikuwa na sarafu aliyoitokea mfukoni mwake kabla hajaondoka. Na, hakika, wakati huo, Rumi ilikuwa ikiitawala Palestina, na fedha zilikuwa ni dinari za Kirumi. Na kwa hiyo walikuwa na sa—sarafu ndogo, mtu angemtupia ombaomba wa kwanza, labda, na hiyo ilitosha kwa siku hiyo. Asingekuwa na uwezo wa ku—kumpa kila ombaomba. Kwa hiyo wa kwanza aliyekutana naye, hakika, aliipata hiyo sarafu. Kwa hiyo walichukua mahali pao nje ya malango, hata kabla ya watu kuingia mjini, watalii, na kadhalika. Nao wakakaa kwenye hilo lango la kaskazini, hasa, wakiwapata watalii waliokuwa wakishuka kutoka kule.

¹⁰ Na kama tunavyoona asubuhi hii tunayozungumzia, jua likianza kupanda juu sasa, yapata saa tatu, yupo ombaomba mmoja aliyefika kidogo amechelewa.

¹¹ Alikuwa na usiku mbaya. Alikuwa ni kipofu. Alikuwa kipofu tangu alipokuwa mvulana mdogo. Naye alikuwa amefika amechelewa. Hakuninii... Alipitiliza usingizi, asubuhi hiyo, kwa kuwa usiku kucha alikuwa akiota ya kwamba angeweza kuona tena. Naye alikuwa amegaagaa kitandani mwake. Na—naye angeweza kuona, aliwazia angeweza kuona, na kuamka akiwa na huku kuvunjika moyo, kwamba asingeweza kuona. Kweli, ilikuwa ni ndoto tu.

¹² Na yeye alikuwa ameshuka akaenda mahali pake. Na alipofika pale, (sasa huu ni mchezo wa kuigiza sasa, kufikia wazo langu) hapakuwapo na mtu pale. Jambo fulani lisilo la kawaida lilikuwa limetukia. Hata hivyo haikuwa imepita saa tatu na nusu ama saa nne, ndipo—ndipo hapakuwapo na ombaomba zaidi pale. Kwa kawaida, kila mtu alikuwa mahali pake. Hakujua kilichokuwa kimetukia mjini; ambacho tulikuwa nacho kwenye kiamshakinywa chetu asubuhi ya leo, na kukizungumzia. Yesu alikuwa ameingia kutoka langoni na alikuwa ameingia mjini, na—na watu wengi walikuwa wameingia wapate kujua yote hayo yalihu nini, nao ombaomba walikuwa wameondoka. Naye hakujua jambo hili, alifika amechelewa. Kwa hiyo tungeweza kumwona wakati alipoanza kuita majina mbalimbali, na hapakuwapo—hapakuwapo na mtu yeyote pale. Kidogo ni hali ya upweke. Alishangaa, vema, huenda ma—maafisa wa Kirumi walikuwa wamewafukuza mahali pale, ama kitu fulani. Kwa hiyo hakumsikia mtu yeyote, kwa hiyo yeye... Kidogo kulikuwa kuna baridi, naye alikuwa na matambara na nguo zake zilikuwa zimechakaa kabisa.

¹³ Ndipo akapapasa-papasa mpaka akapata jiwe lililokuwa huko nje kwenye jua, ambalo labda lilianguka kutoka ukutani wakati Mungu alipoutikisa ule ukuta wa kale ukaanguka, siku za Yoshua. Akaketi juu ya jiwe hili, na alikuwa akijaribu kuwaza kuhusu ndoto yake usiku uliotangulia, jinsi ingekuwa ni halisi kama kweli angaliweza kuona. Lakini, a—asingeweza kuona. Alikuwa ni kipofu. Ndipo akaanza kuwaza juu ya mambo haya, ndipo mawazo yake yakarudi nyuma kwenye ujana wake.

¹⁴ Mwajua, na—napenda kufanya hivyo, kuketi na kuwaza juu ya mambo yaliyopita, mambo mazuri, ya ushindi nilioona Bwana akishinda, na—na hizo nyakati.

¹⁵ Naye Bartimayo, tunavyomjua kwa jina, akiota usiku huo kwamba alifumbuliwa macho, alianza kuwaza jinsi ingekuwa ni halisi kama kweli angeweza kuona. Akawaza, “Loo, nimekuwa kipofu kwa muda mrefu sana, hata sijui jinsi ningejua jinsi ya kwenda huku na huku tena.” Kwa hiyo akaanza kuwazia juu ya miaka mingi iliyopita, wakati alipokuwa mvulana mdogo. Alikuwa akicheza huko juu kilimani, kando yake, ni ufukoni mahali Yordani inaposhukia; nalo bonde liko kule chini, ambamo walikuza nafaka. Na yeye aliishi huko juu kwenye ubavu wa kilima, tutasema. Na akakumbuka jinsi kulivyokuwa kunapendeza, na kwenye majira ya Kuchipua, ku—kuangalia maskini ma—maua wakati yakikua; na jinsi ambavyo angeyachuma makonzi madogomadogo, kisha anaketi na kuangalia mbingu za kupendeza za bluu.

¹⁶ Mnajua, upofu ni kitu cha kuchukiza sana. Ninapomwona mtu, kipofu, moyo wangu unamhurumia. Lakini, hata hivyo, ninajua upofu ulio mbaya zaidi, upofu wa kiroho; jinsi ambavyo Mungu alimuumba mtu apate ku—kumwona Yeye, wala hawawezi kumwona.

¹⁷ Wakati mmoja, kwenye bustani ya wanyama ya Cincinnati, nilikuwa huko chini, sisi na binti yangu mdogo tulikuwa huko. Mimi ninapenda sana mazingira ya porini, kama mjuavyo. Nami niliona walikuwa wamemnasa tai na—na kumweka kwenye kizimba, na maskini jamaa huyo! Nilisikia kelele; nami nilikuwa nimemshika mkono mtoto Sara, na sisi—sisi tukashuka kwenye kizimba hicho. Na hapo ndege huyu mkubwa mno, amejaa damu uso wake wote, manyoya yote yamepukutika. Nikawaza, “Ni tamasha ya kuhuzunisha jinsi gani!”

¹⁸ Akashuka. Akatembea katikati ya kizimba kile. Akaanza, naye huyu hapa anakuja, akipigapiga mabawa yake tena, ku—kugongesha kichwa chake kwenye upande mmoja wa—wa kizimba kile, akipigapiga mabawa yake juu-chini, akijaribu kutoka kwenye kizimba, na kupukutisha manyoya. Bali alikuwa ameshikwa. Akaanguka tena sakafuni akalala pale, ndipo macho yake yakafingirika, akatazama juu na kuona mbingu za bluu ambazo alizaliwa kwa ajili yake. Yeye ni ndege wa

kimbinguni, mnajua. Lakini, mnaona, mafanikio ya maarifa ya mwanadamu yalikuwa yamemweka katika kizimba.

¹⁹ Nilisimama pale nikimwangalia. Nikawaza, “Ningetoa chochote kile kama ningaliweza kumnunua. Kama ningaliweza kumnunua, ningemwachilia, niseme, ‘Nenda zako, jamani, u— utapenda hilo. Ninalipenda pia. Kuwa huru na upae kule juu. Wewe ni wa huko juu. Ulizaliwa kwa ajili ya hilo.’” Nikawaza, “Hiyo ndiyo tamasha ya kuhuzunisha sana niliyopata kuona.”

²⁰ Nikamchukua Sara, nikamshika mkononi mwangu. Nikasema, “Mpenzi, ile pale moja ya tamasha mbaya sana ambayo macho yako yatapata kuangalia.”

²¹ Nikasimama pale, nikiwaza. Nikawaza, “La, na—najua tamasha mbaya zaidi kuliko hiyo. Angalia juu kwenye kilima pale; hao wanaume walioshika kopo la pombe mkononi mwao, wanawake waliovalia kaptura, sigara.” Wakati walizaliwa hasa wapate kuwa wana na binti za Mungu, nao wale pale katika kizimba cha dhambi ambamo Shetani amewaingiza. Watu wa kusikitiwa, vipofu kiroho, waliofungiwa kwenye kizimba; labda ni wafuasi wa kanisa fulani, wanaimba kwenye kwaya, bali hata hivyo wamefungiwa kwenye kizimba.

²² Na kama vile Bartimayo alivyojaribu kuwazia juu ya wakati alipokuwa mvulana mdogo, jinsi ambavyo kwenye saa nane, jioni, maskini mama yake mrembo wa Kiyahudi angemwita, “Bartimayo.” Karibu angeweza kuisikia sauti yake tena, wakati ikitoa mwangwi kote vilimani, naye angekuja mbio. Naye angetoka aende kwenye baraza la mbele na kuchukua kiti cha kale cha kupembea, na kumshika mikononi mwake. Naye akakumbuka jinsi angeyaangalia macho yake mazuri, na jinsi alivyokuwa na mama mrembo. Na jinsi alivyokuwa akimpembeza hata akalala, kwa ajili ya yeye kupata pumziko lake la jioni. Na jinsi ambavyo alifanya hivyo, yeye angemsimulia hadithi, hadithi za watu wao, na za manabii wakuu na wenye nguvu wa Mungu waliokuwa miongoni mwao. Na jinsi alivyopenda hayo, alipenda kuyasikia.

²³ Ni vibaya sana kwamba akina mama wanawaketisha watoto wao kwenye kipindi cha televisheni juu ya kashfa fulani ya Hollywood; badala ya kufanya jambo lile lile, kuwasimulia hadithi za Biblia.

²⁴ Lakini yeye alikuwa mama halisi wa Kiebrania, naye angemsimulia jamaa huyo mdogo hadithi. Angesema, angemwambia kuhusu Mungu kumtuma yule Musa mkuu, mwenye nguvu, wakati walipokuwa ni watumwa huko Misri. Mungu alikuwa amemwahidi Baba Ibrahimu ya kwamba angewakomboa. Ndipo akamtokea na—na—nabii mkuu ambaye Mungu alimwinua miongoni mwao, jina lake Musa. Naye alikuja katika umbo la Nguzo ya Moto, kisha akamtuma Musa huko Misri, na ishara kubwa mno, zenye nguvu na maajabu akawatoa

huko. Na jinsi ambavyo huko nyikani, bila ya mkate wala chochote kile cha kula, hata hivyo walikuwa wakitembea katika utiifu, ndipo Mungu akanyesha mikate kutoka mbinguni.

²⁵ Nami naweza kumsikia maskini Bartimayo akisema, “Mama, hebu kidogo. Hapana shaka Mungu amewafanya Malaika Wake wote kufanya kazi kule juu, na Yeye ana meko makubwa mno ya kuokea huko juu mbinguni, nao Malaika wanafanya kazi ya ziada, wakioka mkate, na kuusukumia kwenye...”

²⁶ “La, kipenzi, wewe ni mdogo sana kuelewa. Unaona, sio lazima Yehova afanye hivyo. Si lazima Yehova awe na meko ya kuokea. Yeye ni muumba. Yeye hunena tu, na ikatokea.”

²⁷ Basi tutasema nini kuhusu Yesu, wakati tunapomwona akichukua kitu kile kile? Hapana budi pana jambo fulani la kiungu kumhusu Yeye. Hapana budi ana uhusiano na Yehova. Mtu fulani leo akijaribu kumfanya nabii tu, ama mtu wa kawaida, ama mwana falsafa, mwalimu mzuri. Yeye hakuwa kitu pungufu ya Mungu aliyedhihirishwa katika mwili.

²⁸ Hapo wakati angezungumza naye na kumwambia juu ya huko kupitia katikati ya—ya—ya ile nyika kuu, ambayo ilikuwa ng'ambo tu ya Yordani wakati huo, na jinsi ambavyo kwenye msimu wa Kuchipua, wakati mwezi wa Aprili, wakati theluji ilipokuwa ikiyeyuka, huko juu katika Uyahudi, na maji yote ya milimani yakitiririka chini, na Yordani yote ilikuwa—ilikuwa imejaa maji, yale maji ya kurudi chini ya vilindi vya mito. Ilionekana kana kwamba Yehova alikuwa ni kiongozi mbaya, kuwapandisha watu Wake kwenye wakati huo ambapo mito ilikuwa imefurika, wakati ikiwa katika hali yake mbaya zaidi. Wangeweza je kamwe kujenga daraja la kuuvuka? Ndiyo maskini Yoshua, ama maskini... si Yoshua.

Bali maskini Bartimayo huenda akasema, “Mama, yeye alifanyaje jambo hilo?”

²⁹ Kasema, “Kipenzi, kumbuka, Yehova angali ni muumba. Yeye alinena tu, na ninii...”

³⁰ Mungu hupenda kuvipata vitu katika...wakati vimeharibika kabisa, na kujionyesha Mwenyewe kuwa ni Mungu. Papo hapo katika msimu wa Kuchipua! Wakati msimu wa Kiangazi, labda ungeweza kuuvuka Yordani kwa urahisi sana pale, kuna kivuko cha maji mafupi kutoka mjini. Tunajua hilo, kwa wapelelezi kwenda kule na kuja kwenye hii. Lakini Mungu aliachilia mabonde yote yajae maji, kisha akaja na kushusha nguvu Zake kuu kutoka Mbinguni na kutengeneza barabara kavu kupitia katikati yake. Palisimama mawe papo hapo chini, ambapo Yoshua aliyakusanya, kama kumbukumbu kwa Yehova, jinsi ambavyo watu wao walivyoshughulikiwa. Naye....

³¹ Nyingine a—aliyoipenda vizuri sana, ilikuwa ni juu ya yu—yule mwanamke Mshunami. Yeye aliikumbuka hiyo. Naye mama yake alikuwa akimsimulia hadithi ya Mshunami, na ya yule nabii mkuu, Eliya, katika siku yake, na jinsi ambavyo mwanamke huyu alikuwa mkarimu kwa huyu nabii. Hata hivyo, yeye hasa hakuwa Mwisraeli. Alikuwa ni Mshunami.

³² Kwa hiyo yeye aliamini kwamba Eliya alikuwa ni nabii, nabii mkuu wa Bwana. Kwa hiyo wakati . . . Siku moja alimwambia mumewe, “Hebu na tumjengee chumba kidogo kando ya nyumba yetu, na tumfadhili, kwa kuwa yeye ni—yeye ni mtu mkuu.”

³³ Na jinsi ambavyo siku moja wakati Eliya na Gehazi, mtumishi wake, walipokuja nao wakaona fadhili hizi zote, yeye alimwambia Gehazi, “Ingia ndani na—na—na ukaulize, “Tufanye nini? Je! niongee na mfalme ama amiri jeshi?”

³⁴ Akasema, “La, mimi nitakaa tu miongoni mwa watu wangu mwenyewe. Ni sawa.”

³⁵ Lakini Gehazi akasema, “Yeye ni tasa. Ni mkongwe, mumewe ni mkongwe, nao hawana watoto.” Kisha akasema . . .

³⁶ Na hapana shaka Eliya aliona ono. Akasema, “Nenda, kamwambie, BWANA ASEMA HIVI, atampata mvulana mdogo.” Na, katika miezi tisa, mvulana huyo mdogo akatokea.

³⁷ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . mkubwa, yeye alikuwa pamoja na baba yake, huko nje shambani, wakivuna, na hapana shaka alishikwa na ugonjwa kutokana na jua kali. Akashika kulia, “Kichwa changu! Kichwa changu!” Ndipo baba akampeleka nyumbani. Mama akamweka mapajani mwake, akampembeza, na labda akampa dawa zote zilizokuwamo za kumpa. Naye maskini mtoto huyo akazidi kuugua mpaka, hatimaye, mnamo adhuhuri, akafa.

³⁸ Na jinsi ambavyo maskini mama huyo asingeweza kushindwa! Baba alipoingia ndani, na majirani wote wakaingia, nao walikuwa wakiomboleza na kupiga mayowe, maskini jamaa mdogo amekufa, lakini yeye angali alikuwa na imani kwa huyu nabii, nabii wa Kiebrania; yeye, Mmataifa. Akasema, “Nitandikie nyumbu, na—na usininii—usinini—usisimame, bali acha niende kwenye lile pango anamoishi huyu nabii, juu ya Mlima Karmeli.”

³⁹ Ndipo mumewe akasema, “Sio mwandamo wa mwezi wala sabato, naye hatakuwapo.”

Akasema, “Ni sawa.”

Akasema, “Haya nenda.”

⁴⁰ Ndipo Eliya alipomwona akija, yeye na Gehazi walitoka pangoni, wakaangalia, wamesimama hapo nje. Naye huyu hapa anakuja. Akasema, “Huyu hapa Mshunami anakuja, naye ana huzuni, bali Mungu amenificha hilo, kwa moyo wangu.”

41 Mnajua, Mungu hawaambii manabii wake kila kitu, kile tu anachowataka kujua.

42 Kwa hiyo a—akaangalia, kisha akasema, “Yeye ni...” Kasema, “Nenda, kamlaki, ukaseme, ‘Hujambo? Mume wako hajambo? Mtoto wako hajambo?’”

Na hii ndiyo sehemu ninayoipenda, pia.

43 Wakati Gehazi alipomlaki, alisema, “Hujambo? Mume wako hajambo? Mtoto wako hajambo?”

44 Akasema, “Hawajambo.” Mtoto mchanga amekufa, mume anaomboleza, machozi yakitiririka moyoni mwake, lakini, “Hatujambo.” Alikuwa amekuja mbele ya mtu ambaye angeweza kumwambia na kumbariki, na, alikuwa na mtoto mchanga, hakika Mungu angefunua ni kwa nini Yeye alimchukua. “Bwana alitoa, Bwana ametwaa, Jina la Bwana libarikiwe!” Alitaka kujua ni kwa nini.

45 Halafu jinsi ambavyo alikuja na kusujudu miguuni pa Eliya, naye Gehazi akamwondoa upesi; hilo halikumfaa bwana wake. Naye akafichua shida yake. Ndipo Eliya akaenda huko na kumfufua mvulana huyo mdogo, kwa kuulaza mwili wake juu ya jamaa huyo mdogo.

46 Nami ninawatakeni muione imani ya mama huyo, pia. Alimlaza mtoto huyo mchanga juu ya kitanda ambacho Eliya alikuwa anakilalia. Ninawatakeni mninii. . .

47 Ninataka kuliweka wazi wazo la Paulo hapa, jinsi niwazavyo mimi. Mwajua, Paulo aliweka leso juu ya wagonjwa na wanaoteseke, na nguo. Siamini ya kwamba Paulo aliyakiuka Maandiko. Nafikiri hapa ndipo alipolipata. Mnakumbuka jambo la kwanza Eliya alilomwambia nanii—Gehazi? “Chukua fimbo yangu ukaiweke juu ya mtoto huyo.” Yeye alijua kila kitu alichokigusa kilibarikiwa. Na kwa hiyo, mnakumbuka, Paulo hakuziombea leso hizo. Walizichukua tu kutoka mwilini mwake. Hiyo ilikuwa ni imani ya watu hao.

48 Kwa hiyo, unaona, yeye alisema, “Itwae fimbo yangu na (mtu akikusalimu, usimjibu) kaiweke juu ya mtoto huyo.”

49 Lakini imani ya mwanamke huyo haikuwa kwenye fimbo hiyo; ilikuwa katika nabii. Basi akasema, “Sitakuacha mpaka . . . Hakika kama nafsi yako iishivyo, si—sitakuacha.”

50 Kwa hiyo Eliya, apate kumwondosha, ilimbidi aambatane naye. Kwa hiyo aliingia na kujilaza juu ya maskini mtoto huyo mchanga, aliyekufa, ndipo akapiga chafya mara saba na akafufuka.

51 Jamani, hiyo—hiyo ilikuwa ni hadithi ya kupendeza jinsi gani kwa maskini Barti- . . . Bartimayo, wakati alipokuwa mvulana m—m—mdogo. Jinsi alivyoipenda hiyo hadithi ndogo, kwa maana ilikuwa ni kufufuliwa kwa mvulana mdogo. Hiyo ilikuwa ni moja ya alizozipenda sana.

⁵² “Lakini hiyo ilikuwa ni katika siku zilizopita,” kuhani anamwambia sasa. “Ole, hizo zilikuwa ni zile siku ambapo Israeli walikuwa na watu wakuu, wenye nguvu; manabii wakuu, wenye nguvu walipotembea nchini.” Lakini makuhani wakasema, “Mwajua, Yehova hawahitaji manabii tena.” Si makuhani pekee wanaosema hilo. Lakini—lakini walisema wakati huo, “Yehova hahitaji manabii tena. Yeye alitupa torati, nasi tukajenga kanisa, hekalu, na hilo tu ndilo tunalohitaji.” Na ni karibu tu na vile wanavyoliamini leo hii, bali Yehova angali ni Yehova wala hawezi kubadilisha njia Yake; Yeye ni Mungu, wala hana kigeugeu. Sasa wao waliamini kwamba hilo—hilo tu ndilo wa—walilohitaji.

⁵³ Na kwa hiyo wakati alipokuwa ameketi pale katika ndoto hii ya mchana, kama ilivyokuwa, akiwazia, nayo macho yake mapofu yameinuliwa kuelekea kwenye jua kali; mara, anasikia vishindo vya miguu ya maskini nyumbu mdogo akishuka kwe—kwenye barabara iliyojaa mawe, akishuka kutoka Yerusalemu, mawe yaliyotandazwa, akiingia. Wakati, basi akasikiliza kwa makini, na alikuwapo mtu aliyevaa makubadhi akikimbia mbele ya maskini nyumbu yule. Naye alijua hapana budi huyo ni tajiri, kwa sababu alisafiri kwa nyumbu na pia alikuwa na mtumishi aliyemwongoza nyumbu huyo.

⁵⁴ Kwa hiyo anasimama, akijua ya kwamba ilimbidi kupata fedha apate ku—kuishi. Kwa hiyo anasimama na kujifunika vazi lake, na maskini vazi kuukuu, na kukimbia kuelekea mtaani, ndipo akasema, “Ningetaka sadaka. Nilichelewa asubuhi ya leo. Waweza kunipa sadaka tafadhali? Mimi ni kipofu.”

⁵⁵ Nasi tunasikia sauti kali sana ikija, “Simile, ewe ombaomba! Mimi ni mtumishi wa Yehova. Mimi ni kuhani. Ninashuka kutoka Yerusalemu, nimetumwa na shirika, kuukomesha huo mkutano wa uponyaji utakaofanyiwa hapa chini asubuhi ya leo Ye—Yeriko. Inanibidi kukutana na ndugu hapa chini tuhakikishe kwamba kitu hicho hakiendelei, tuwapate watu. Kuna nabii wa uongo nchini, unaona. Tunaninii...tunasikia yuko Yeriko asubuhi ya leo, nami niko njiani mwangu. Simile!” Kuhani. “Basi, vema, ewe mtumishi, nenda zako.” Ndipo maskini yule nyumbu akaenda shoti tena.

⁵⁶ Ndipo ombaomba huyo anaenda zake akipapasa-papasa mpaka akalipata lile jiwe, akaketi. Akaendelea na ndoto zake, na wakati alipoanza kuwaza, “Huko nje kwenye ile barabara ndogo nilipokuwa nimesimama; sio muda mrefu sana uliopita, yule nabii mkuu na mwenye nguvu, Eliya na Elisha, walikuja, wameshikana mikono, wakitembea kwenye barabara hiyo hiyo, wameshikana mikono, wakashuka kwenda Yordani. Nayo Yordani ilikuwa ifunguke tena. Na ng’ambo ya pili, kwa ajili ya huyu nabii mzee mchovu, Eliya, kulikuwako na gari la Moto na farasi wa Moto, wamefungiwa kwenye tawi fulani pale, wapate kumpeleka nyumbani. Naye alikuwa alione jambo

hili, kijana Eliya. Elisha alipaswa kuangalia nyuma na kuona huduma mbele zake, kile kilichowekwa mbele zake. Ilimbidi kumkazia macho huyu nabii.”

⁵⁷ Nami ningewazia Bartimayo alisema, “Laiti ningaliishi kwenye siku hiyo, na nilikuwa nimeketi hapa, ningaliwakimbilia hao manabii, nianguke kifudifudi, na kusema, ‘Ee, nabii wa Mungu! Niombee, na Yehova atanifumbua macho yangu tena.’ Lakini kuhani anasema, ‘Hiyo ni, hakuna kitu kama hicho tena. Hatunacho hicho. Yehova haponyi kwa nguvu Zake, tena. Tunao madaktari na kadhalika wanaofanya hayo. Wala hatuhitaji hayo tena, kwa hiyo Yehova haponyi. Huo ulikuwa ni wa siku iliyopita. Sisi tunashika tu torati. Nasi hushikwa na ugonjwa, ndipo tunakufa na kwenda Mbinguni, na hakuna lingine. Hayo tu ndiyo tunayohitaji.’”

⁵⁸ Basi alipoanza kuwaza, ndipo akakumbuka. Si yadi mia tano kutoka mahali alipokuwa ameketi; Israeli wakiisha kuvuka na kupiga kambi, na yote yakiwa katika utaratibu, mahema yote mahali pao, wakingojea amri kwenda kiaskari mpaka Yeriko. Na labda jiwe lile lile alilokuwa amelikalilia lilikuwa ambalo Yehova alikuwa amelilipua ku—kutoka kwenye kuta zile.

⁵⁹ Ndipo akasema, “Wazia tu jambo hilo! Sio muda mrefu sana uliopita, shujaa mwenye nguvu, Yoshua, mtumishi mkuu wa Mungu, mwenye nguvu, aliuvuka ule mto, kwenye majira ya Kuchipua, akapiga hema, papo hapo mbele ya adui. Siku moja, wakati akisoma mbinu zake za shambulizi la Yeriko, jioni moja wakati akitembea huko nje, ama asubuhi moja, akiyakagua malango kote kote, na jinsi yalikuwa ni makubwa. Wangeweza kufanya mashindano ya magari juu yake, farasi, kadhaa wakienda sambamba, kulizunguka lango. Jinsi Yoshua alivyokuwa akiangalia. Aliangalia kuegemea ukuta, na pale amesimama Mtu ameuchomoa upanga Wake. Yoshua akauchomoa upanga wake akamwendea. Yoshua akapaza sauti, akasema, ‘Wewe u upande wetu au Wewe ni mmoja wa adui zetu?’ Yeye akasema, ‘La, Mimi ni Amiri wa jeshi la Bwana.’ Yoshua mwenye nguvu akatupa upanga wake chini, akatoa chapeo yake na akaanguka miguuni Pake.”

⁶⁰ Kipofu Bartimayo akiwazia, “Hiyo haikuwa ni yadi mia tano kutoka mahali ninapoketi sasa hivi. Ambapo jeshi lenye nguvu la Bwana, Amiri jeshi, na Yoshua akasujudu miguuni Pake. Loo, laiti ningalikuwa tu pale kwenye hayo mahema, kipofu wakati huo, ningalimwomba Amiri jeshi mwenye nguvu wa jeshi la Bwana kama angeweza kunifumbua macho, na Yeye angalifanya hivyo.” Hakujua ya kwamba Amiri jeshi yuyo huyo alikuwa umbali usiofikia yadi mia moja kutoka kwake.

⁶¹ Hapo ndipo tunapokosea, usiku wa leo. Tunajaribu kuweka utukufu wote, na Kristo, huko nyuma kabisa kwenye wakati mwingine. Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

Yupo hapa kwenye jengo hili, usiku wa leo, kadiri alivyowahi kutembea Galilaya ama Yerusalemu.

⁶² Huyu Amiri jeshi mkuu alikuwa akitoka nyumbani mwa Zakayo, nao watu walikuwa—walikuwa wakimngojea nje.

⁶³ Katika dakika chache, anasikia uvumi, na uvumi huo una sauti iliyochanganyikana.

⁶⁴ Mmoja anasema, “Hosana kwa Nabii ajaye katika Jina la Bwana! Heri aliye Nabii wa Galilaya, Mtumishi wa Yehova!”

⁶⁵ Wengine walisema, “Hatumtaki Mtu kama huyo! Hatutakuwa na lolote la Huyu hapa mjini.” Na huku wakija, na baadhi yao wakimtupia matunda yaliyooza, wakati akipitia langoni.

⁶⁶ Na yeye—yeye hakuwa amesikia kitu kama hicho, kwa hiyo akasema, “Ni kitu gani kinachoendelea? Uvumi huu wote unahusu nini? Kuna nini huku?” Nao watu wakisongamana.

⁶⁷ Baada ya kitambo kidogo akaisikia sauti ya kuhani yule aliyeshuka kulifanya shirika lisiuruhusu mkutano huo. Akamsikia akisema, “Wananiambia ati Wewe huwafufua wafu. Sasa tuna sehemu nzima ya makaburi iliyojaa hao hapa juu kilimani, hebu na tukuone ukija huku na kuwafufua wengine mbele zetu.”

⁶⁸ Lakini, mnajua, Yeye alikuwa akielekea Yerusalemu, akikwea kwenda kusulibishwa. Dhambi zote za ulimwengu zilikuwa juu Yake, Naye alikuwa akienda Yerusalemu akatolewe dhabihu. Nao walimdhihaki na kumfanyia mzaha; na baadhi yao wakimbariki, na wengine wao wakimlaani. Kama tu ilivyo kwenye karibu kila mkutano alipo Yeye; baadhi wako upande Wake, wengine wanamchukia. Lakini ilionekana kuwa haikumsumbua Yeye. Alikuwa ameelekeza uso Wake kwenye mwisho wa kazi Yake. Naye anakaza mwendo, kwa utaratibu, akienda zake, akielekeza macho yake Yerusalemu. Na maskini watu kumi na wawili walikuwa wamemzungushia ukuta pale, wakijaribu kuuzuia umati. Huku wengine wakijaribu kumgusa. Na wengine wakipaza sauti na kumdhihaki, na—na kadhalika.

⁶⁹ Nao umati huo karibu umkanyagie chini maskini kipofu huyo, mhusika wetu tuliye naye usiku huu, nao walikuwa wamemsukuma wakamwangusha. Basi hebu tuwazie ya kwamba palikuwapo na maskini msichana mdogo, mzuri aliyepitia hapo, huenda ikawa labda alikuwa ni dada ya Rebeka kwenye hadithi yetu asubuhi ya leo, ama alikuwa ni mwa—mwaminio wa Kristo. Naye aliwaona wakimsukuma huyo mzee, na alipoona ya kwamba alikuwa...hawakumhurumia. Lakini kwa kuwa yeye alikuwa mwaminio wa Yesu, lilimfanya kuwa na huruma. Daima hufanya hivyo. Linakufanya kuyajali masilahi ya wazee na maskini. Basi maskini mzee huyo alikuwa amesukumwa akaangushwa chini, naye akainama amchukue. Akaninii...

70 Huenda alimwambia, kitu kama hiki, “Msichana, natambua, kwa sauti yako, wewe ni msichana.”

71 “Naam, ndivyo. Mzee, waweza kusimama? Ninaamini wanaweza kukuumiza.”

72 Akasema, “Vu—vurugu hili lote ni la nini? Mahangaiko haya yote, mahangaiko haya ni ya nini? Haya yote yanahusu nini?”

73 “Mbona,” akasema, “hivi hujafahamu ya kwamba Yesu wa Nazareti, Mwana wa Daudi, yumo mjini? Huyu ni Yeye akipita hapa, Nabii wa Galilaya. Unataka kusema ati hujui?”

“La, si—si—sijapata kusikia habari Zake.”

74 “Vema, hebu nikwambie lililotukia asubuhi ya leo mjini. Hivi unamjua Zakayo, yule mtu wa mkahawa?”

“Naam.”

75 “Sikuzote kwa namna fulani amekuwa mkosoaji. Mke wake alikuwa ni mwaminio. Na asubuhi ya leo, Zakayo, akiwa juu mtini, kumwangukia Yesu akipita. Na sote tunajua ya kwamba Yeye ni Nabii. Ndipo alipopitia pale, Yeye alisimama na kuangalia juu na kumwita Zakayo kwa jina lake; kamwe hajakuwako Yeriko hapo awali.”

76 Mzee huyo ombaomba akachangamka. Akasema, “Basi hilo ni timilizo la Kumbukumbu la Torati 18:15, ‘Bwana Mungu wetu atatuondokeshea nabii kama Musa.’ Huyu hana budi kuwa ni Yeye. Kama Ndiye, Yeye yuko wapi sasa?”

“Yeye yuko kama yadi mia moja huku chini barabarani.”

77 Tayari amempita, akawaza. Kwa hiyo akaanza kupaza sauti, “Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu. Unirehemu, Ee Mwana wa Daudi. Unapopitia hapa, unirehemu.”

78 Sasa, kimwili, Yeye asingaliweza kuisikia sauti yake, kwa sababu ya vurugu hilo lote. Wengine wakimsifu na wengine wakimbariki, na wengine wakimlaani. Na, vurugu hilo, kamwe a—asingalimsikia.

79 Lakini Yeye alikuwa ni Neno. Na wakati nafsi inapolia; kama vile yule mwanamke aliyetokwa na damu, ambaye aliligusa vazi Lake. Biblia ilisema, “Akasimama kimya.” Ilimsimamisha. Liwazie jambo hilo, liwazie tu jambo hilo; kwamba wi—wito wa mzee huyo mmoja ombaomba, asiye na maana, huku akiwa na dhambi za ulimwengu na amejitwika mzigo, akienda Yerusaelu apate kuwa toleo la dhambi, hata hivyo wito wa mtu mmoja ulimfanya kusimama kimya.

80 Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Wito mmoja, usiku wa leo, utamleta jukwaani, kama tu vile ulivyofanya wakati huo. Jinsi ambavyo anabaki Yeye yule!

81 Ninakumbuka, usiku mmoja nikija kutoka Dallas, Texas. Imekuwa ni miaka kadhaa iliyopita. Ndege yetu ilizuliwa kuruka hu—huko Memphis. Nao wakaniweka kule juu kwenye

ile hoteli inayojulikana sana, shirika hilo la ndege liliniweka, Peabody Hotel. Nao wakaniambia wageniita kesho yake asubuhi, wakati mzuri kuchukua limosini, kurudi kwenye hiyo ndege.

⁸² Nami nilikuwa nimelala vizuri usiku kucha; nikaamka kesho yake asubuhi, nikiwa nimeandika barua chache, nilikuwa nikishuka kwenda posta, kuzituma. Nilitoka nikaanza kwenda zangu barabarani. Na mara, nikasikia kitu Fulani kikisema, “Simama, na urudi nyuma.”

⁸³ Vema, mwajua jinsi watu hupata dhana. Nami nikawaza, “Vema, labda hilo ndilo.”

⁸⁴ Nikaenda mbele kidogo, nayo ikaendelea kusema tena, “Simama, na urudi nyuma.”

⁸⁵ Vema, ni—nikaenda pembeni, kulikuwako na polisi Mwairishi mnene pale pembeni, nami sikuninii... Nilikuwa nikiangalia vigurudumu vya kuvulia samaki na kadhalika, dirishani. Na huenda kidogo nilisimama kwa muda mrefu kupita kiasi naye huenda akanituhumia kwamba nilikuwa nikijaribu kuchukua moja ya vigurudumu hivyo, kwa hiyo niligeuka tu na kuanza kurudi. Na wakati nilipokuwa nikirudi, upesi, upesi, na nikapitia papo hapo hotelini, na nikashuka kuelekea upande wa mto, huko chini sana. Sijui, nadhani ningeweza kupapata mahali hapo, usiku wa leo. Ndipo nikawaza, “Hapa inachelewa, lakini kitu Fulani...”

⁸⁶ Je! mnaamini kuongozwa na Mungu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Na wakati nikiendelea na safari, ni—ni... Kulikuwa kunachelewa na nilijua ilinibidi kuharakisha, bali kitu Fulani kiliendelea kusema tu, “Endelea, endelea.”

⁸⁷ Na wakati nilipofikia ambapo nimechelewa sana kurudi na kuipata ndege yangu, niliwaza, “Vema, si—sina budi kuufuata mwongozo huu.” Na ilitokea nilikuwa nikiimba wimbo huu mdogo, niliokuta tu nanyi Wapentekoste, kuhusu:

Walikuwa wamekusanyika katika chumba cha
juu,
Na wote wakiimba katika Jina Lake,
Na kubatizwa katika Roho Mtakatifu,
Ndipo nguvu za huduma zikaja.

⁸⁸ Mlipata kuusikia huo wimbo? “Na ninafurahi ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.” Nilikuwa nikijaribu kuurudia huo tena, nikisema:

Njoo, ndugu yangu, itafute baraka hii
Itakayousafisha moyo wako kutokana na
dhambi.

⁸⁹ Na wakati nilipoendelea mbele, nikishuka mtaani, niliangalia, na palikuwapo na maskini Shangazi Jemima wa kawaida ameegemea juu ya ua dogo, na maskini, nyumba ya

mtu mweusi pale, iliyo fanana na kibanda kidogo, kilichopakwa chokaa, akiegemea juu ya ua. Alikuwa amejizungushia shati la mwanamume kichwani.

⁹⁰ Ndipo nikaacha tu kuimba na kuanza kwenda mbele. Sikujua nilikokuwa nikienda; Yeye alisema tu, “Endelea, endelea tu kutembea.” Na kwa hiyo nilipomkaribia sana, niliona kidogo alikuwa akitabasamu. Ndipo nikamwanguka, kisha nikageuza kichwa changu na kuendelea na safari.

⁹¹ Akasema, “Habari za asubuhi, mchungaji.” Sasa, huko Kusini, *mchungaji* linamaanisha “mhudumu.”

Nami ni—nikasema, “Njema, shangazi.”

⁹² Nikaangalia nyuma, nami nikawazia, “Hivi alijua je mimi ni mchungaji?” Hata sikuwa na Biblia wala chochote kile.

Nikageuka. Nikasema, “Ulijuaje mimi nilikuwa mchungaji?”

Akasema, “Nilijua ulikuwa unakuja.”

Nami nikasema, “Kidogo ni jambo lisilo la kawaida, kwangu.”

⁹³ Na—na yeye akasema, “Hivi ulipata kusoma katika Biblia juu ya yule mwanamke Mshunani?”

Nikasema, “Loo, ndiyo, mama.”

⁹⁴ Akasema, “Unajua, hakuninii; alikuwa ni tasa, asingeweza kupata watoto.”

Nikasema, “Naam, mama, ninaikumbuka hadithi hiyo.”

⁹⁵ Kasema, “Naye alimwahidi Bwana, na alikuwa atamlea mtoto huyo kwa Bwana, hakika.” Kisha kasema, “Unajua, nilikuwa mwanamke wa aina hiyo.” Akasema, “Nisingeweza kupata watoto, mimi na mume wangu.” Ndipo akasema, “Nilimwahidi Bwana, kama atanipa mtoto, ya kwamba ningemlea kwa ajili Yake.” Kasema, “Yeye alinipa mtoto.” Na akasema, “Nilimlea mvulana huyo vizuri nilivyoweza, kumtumikia Bwana.” Akasema, “Lakini, unajua,” akasema, “aliingiana na kundi baya, naye akaambukizwa u—u—ugonjwa mwilini mwake.” Kisha kasema, “Mtu daktari tayari amemdunga sindano zote anazoweza kumdunga. Na tayari umeingia ndani,” kasema, “damu yake ni zaidi ya nne, ugonjwa wa zinaa,” kaswende. Na kwa hiyo kasema, “Sehemu ya damu yake inatiririka inarudi kupitia moyoni mwake. Moyo wake una mashimo ndani yake.” Ndipo kasema, “Yeye amelala mle ndani, hajisikii.” Kisha kasema, “Mtu daktari alikuwa hapa, siku mbili zilizopita, na kusema, ‘Hataamka tena. Amekwisha.’”

⁹⁶ Kisha kasema, “Kamwe siwezi kuvumilia kumwona mtoto wangu mchanga akifa namna hiyo.” Na kasema, “Basi ni—ni—niliomba usiku kucha, ‘Bwana, kama utamchukua... Ulinipa; bali na—na—nataka kumsikia akisema ameokoka, ndipo nitajua

nitakutana naye tena.” Kisha kasema, “Ni—niliomba, na nikaomba ombi ambalo nilimtaja yule mwanamke Mshunami.”

⁹⁷ Ndipo akasema, “Ni—nilienda kulala, nami nikaota ndoto.” Akasema, “Nami nikamwambia Bwana, kasema, ‘Wewe ulinipa mtoto huyu mchanga.’ Na kasema, ‘Nilikuwa kama yule mwanamke Mshunami, bali yuko wapi nabii Wako?’ Pia kasema, Yeye akasema, ‘Angalia, akija hapa.’ Ndipo nikamwona mtu mwenye kofia ndogo imewekwa upande mmoja wa kichwa chake, amevaa hiyo suti ya kijivu, akishuka mtaani.”

⁹⁸ Kisha kasema, “Hiyo ilikuwa ni kama saa kumi usiku huu.” Akasema, “Nimesimama hapa tangu wakati huo.”

Yeye angali ni Mungu. Yeye hujibu pande zote mbili.

⁹⁹ Nikasema, “Jina langu ni Branham. Mimi huwaombea wagonjwa. Ulipata kusikia habari za huduma yangu?”

¹⁰⁰ Akasema, “La, bwana, Mchungaji Branham, kamwe sijasikia habari zako.” Kisha akasema, “Hutaingia ndani?”

¹⁰¹ Ndipo nikaanza kulifungua lango. Kulikuwako na uzio mdogo wa zamani pale, nalo lango hilo lilikuwa na kisahani cha plau kimening’inia juu yake, kama ilivyo huko Arkansas. Ilikuwa tu ni ng’ambo ya mto kutoka kwake, hata hivyo, kwa hiyo mnajua hiyo ilikuwa ni nini. Kwa hiyo nikarudisha lango nyuma nikaingia ndani.

¹⁰² Wakati nilipoingia kwenye nyumba hiyo. Nimekuwa katika majumba ya wafalme, wafalme watatu ama wanne mbalimbali; mfalme wa Uingereza, Mfalme Gustav wa Sweden, mahali pengi, kuingia na kuwaombea. Nami nimekuwa katika baadhi ya nyumba zilizo nzuri sana, nadhani, huko Hollywood. Lakini kamwe sikukaribishwa vizuri zaidi kuliko nilivyokaribishwa huko. Maskini chumba kidogo tu cha kawaida, vyumba viwili, jiko dogo huko nyuma, chumba kidogo cha kulala hapa, na kitanda cha kale cha posta. Hakukuwapo na vibandiko ukutani. Lakini kulikuwako na maandishi pale, yaliyosema, “Mungu yabariki makazi yetu.”

¹⁰³ Nikaangalia, mvulana mkubwa mno wa kinegro, amelala pale, alionekana kana kwamba yuna umri wa miaka kumi na minane, mvulana mkubwa, mwenye nguvu, aliyeonekana mwenye afya. Naye alikuwa ameshika blanketi, na alikuwa akikoroma, “Uhu! Uhu!”

Ndipo nikasema, “Kwani ana shida gani?”

¹⁰⁴ Akasema, “A—anafikiri yuko huko nje kwenye bahari yenye giza, amepotea. Naye anasema, anaendelea kusema ya kwamba ame—potea, huko baharini,’ na haoni njia. Anafikiri anapiga mtumbwi makasia.” Kasema, “Amekuwa akifanya hivyo kwa siku mbili ama tatu.” Kisha kasema, “Si—siwezi kabisa kumwacha afe jinsi hiyo.” Kasema, “Je! utamwombea?”

Nikasema, “Naam, mama.”

105 Nikaanza kuzungumza juu ya uponyaji. Hakuwa na hamu ya huo. Yeye alitaka tu kusikia akisema alikuwa ameokoka. Hilo tu ndilo alilokuwa na hamu nalo, kwamba alikuwa ameokoka. Nami ni—nikasema yeye ni . . .

106 Akaenda pale akamshika kichwani na kumvuta nyuma, akambusu shavuni, na akasema, “Mungu ambariki kipenzi cha mama.”

107 Mimi nikisimama pale nikiangalia hilo, nami nikawaza, “Naam, naam, jambo ndilo hilo.” Haidhuru aliiletea familia aibu jinsi gani, ameenda umbali gani, haidhuru ameingia kwenye shida gani, yeye angali ni “mtoto mchanga wa mama.”

108 Ndipo nikawaza, “Biblia ilisema, ‘Mama anaweza kumsahau mtoto wake anayenyonya, bali siwezi kuwasahau. Ninyi ni . . .’ Ni upendo jinsi gani uliopo! ‘Majina yenu yamechorwa katika vitanga vya mkono Wangu.’”

109 Akambusu. Tukapiga magoti. Nikaketi upande wa chini wa kitanda. Nikaweka mikono yangu juu ya miguu yake, ilikuwa na joto, inanata.

110 Nami ni—nikasema, “Shangazi, utaomba kwanza?” Na, rafiki yangu, nilijua alikuwa amesema Naye hapo awali. Loo, ni ombi la jinsi gani alilomba kwa Mungu!

Ndipo akasema, “Waweza kuomba?”

Nami nikasema, “Naam, mama.”

111 Nikasema, “Baba wa Mbinguni, nimechelewa angalau saa moja kwa ile ndege. Uliniambia ni—nije huku, na niendeleo tu kuja. Halafu sijui kama hapa ndipo ulipunitaka, ama sivyo, bali hapa ndipo nimesimama. Kama ulinituma kumwomba mvulana huyu . . .”

112 Na yapata wakati huo, yeye akasema, “Loo, mama!”

Akasema, “Kipenzi cha mama anataka nini?”

113 Kasema, “Nuru inaingia chumbani.” Kama dakika tano, alikuwa ameketi kitandani.

114 Nikakimbia nje, nikashuka. Nikawaza, “Vema, ninaweza tu kuchukua teksu, hivyo tu, na kungojea zaidi ya siku moja, ama wakati wowote ninaoweza kupata ndege nyingine.”

115 Hapo nilipokuwa nikiingia langoni, nimechelewa saa mbili na kitu, nikamsikia akisema, “Wito wa mwisho wa ndege namba sitini na saba, kwenda Louisville, Kentucky.”

116 Ati nini? Ati nini? Ukuu wa Mungu! Mnaona? Maombi na imani ya mwanamke huyo maskini wa kinegro, asiye na maana, iliizuia hiyo ndege na kuishikilia hapo. Yeye ni Mungu yeye yule ambaye angeweza kusimama na kumgeukia ombaomba kipofu kwenye—kwenye kuta za Yeriko. Ni Mungu yeye yule jana, leo, na hata milele. Imani ndiyo inayofanya jambo hilo. Yeye anakutaka uliamini.

¹¹⁷ Jambo lingine, kama miaka miwili baadaye nilikuwa nikipitia pale kwa garimoshi, nikienda, nikirudi Phoenix. Na, mwajua, wanakuuzia hizo sandiwichi kwa bei ya juu sana, mimi hujaribu kushuka kwenye stesheni na kujinunulia hambaga kadhaa, kifurushi kizima chake, nitakazotumia mpaka nitakaposhuka, maana wanakulipisha senti sabini na tano kwa maskini sandiwichi ndogo ambayo imekatwa ndogo sana hata ina upande mmoja tu. Na—nayo, sasa, ni mbaya sana. Ndipo ni—nikaruka nje nilipofika Memphis. Na kama mtu yeyote aliwahi kuwa huko Memphis, anajua jinsi ambavyo garimoshi linavyoingia kwenye jukwaa la kugeuzia hapa. Niliruka nikatoka na kushuka huko chini upesi kwenye kibanda cha hambaga.

Nikamsikia mtu fulani akisema, “Aloo hapo, Mchungaji Branham!”

¹¹⁸ Nikaangalia kote, huyu hapa maskini mbeba mizigo amesimama pale, amekiinua kichwa chake. Nikasema, “Aloo, mwanangu,” nikaanza kurudi.

Kasema, “Wewe, wewe hunijui mimi, sivyo?”

Nikasema, “La, siamini ninakujua.”

¹¹⁹ Kasema, “Unajua, siku moja ulikuja nyumbani kwangu.” Kisha kasema, “Mama yangu alikuwa amesimama huko nje, nawe ukampapasa mgongoni, amelowa maji.”

Nikasema, “Wewe si yule mvulana?”

¹²⁰ Kasema, “Naam, ndo mimi.” Akasema, “Naam, mimi—mimi ndo yule mvulana.” Akasema, “Si kwamba tu ni—nimeponywa,” lakini kasema, “ni—ni—nimeokoka tangu wakati ule, pia.” Kwa hiyo, hivyo, ndivyo ilivyokuwa.

¹²¹ Loo, neema ya ajabu! Mungu yeye yule, ambaye ombaomba kipofu angeweza kumsimamisha, maskini mwanamke wa kinegro, asiye na maana, angeweza kuizuia ndege. Maombi yake na imani katika Mungu! Alikuwa akiamini.

¹²² Yesu alisimama kimya. Uso wa yule ombaomba kipofu ulimsimamisha papo hapo njiani Mwake ningetaka kuwa na siku chache usiku, kuhubiri juu ya somo hilo, “Ndipo basi Yesu akasimama kimya.” Lakini huyo hapo amesimama, kasema, “Mleteni hapa.” Amina.

¹²³ Nilikuwa nikisoma hadithi kuhusu kipofu Bartimayo, hapa wakati fulani uliopita, wakati nilipokuwa nikiisoma historia ya Biblia. Labda ni hekaya, bali ilisema ya kwamba daima aliamini katika uponyaji. Haidhuru makuhani walisema nini, yeye angali aliuamini. Kasema alikuwa ni mtu aliyekuwa ameo, alikuwa na mke, na msichana mdogo ambaye kamwe hakuwa amemwona. Alikuwa karibu ni wa huo umri wakati huo, kama umri wa miaka kumi na sita. Kamwe hakuwa amemwona. Kasema kile alichofanya kwa ninii—ninii . . .

¹²⁴ Mwajua, huna budi kuwa na kitu cha tofauti kidogo na jamaa huyo mwingine, wakati ukiomba, vinginevyo huwezi kuvutia watu. Huko India, wa—wanaacha maskini hawa nguchiro wadogo kumuua swila, na chochote kile wanachoweza kufanya kuwavutia watu. Nimemwona tu—tumbili akichukua kijiti na kuuchapa tu mpira, mtaani, kitu chochote kile, kuwavutia watu, ndipo wanawapa fedha.

¹²⁵ Nayo ilisema Bartimayo alikuwa na hua wawili wadogo ambao wangepanya, wangepanya sarakasi, kama ninii mdogo... mmoja juu ya mwingine, na hiyo iliwatumbuiza wa—watu, watalii, nao wangempa fedha.

¹²⁶ Nayo ikasema usiku mmoja mke wa—wake alikuwa mgonjwa sana. Nao walikuwa na daktari, naye daktari akasema, “Bartimayo, hakuna kitu ninachoweza kufanya. Yeye, siwezi kuimaliza homa hiyo.”

¹²⁷ Na ilisema alipapasa akaenda zake ukutani, akatoka nje ya nyumba, na kusema, “Yehova, ninakupenda. Ninakuamini. Sina kitu ninachoweza kukutolea. Nina hua wawili wadogo hapa, ninaojipatia riziki yangu kwao. Lakini kama utamruhusu tu mke wangu mpendwa akae pamoja nami na kunisaidia kumlea mtoto wangu; nami ni kipofu, wala siwezi kuona; kama Wewe utamruhusu tu mke wangu apone kusudi aweze kunisaidia hapa na pale, nitakuahidi, kesho nitatoa sadaka kubwa. Nitawachukua maskini hua wangu wadogo huko, kama sadaka ya matoleo yangu.”

¹²⁸ Vema, wanasema mke wake alipona. Akawachukua hua hao na kuwatoa sadaka.

¹²⁹ Wakati fulani baada ya hapo, msichana wake mdogo akawa mgonjwa. Yeye pia alikuwa mahututi, kwa hiyo akaenda kuomba tena. Akasema, “Yehova, sina chochote kilichosalia, bali nina mwana-kondoo wangu.” Na katika siku hizo, mwana-kondoo alimwongoza kipofu kama vile mbwa wa jicho la kuona anavyofanya sasa, walifunzwa kuwaongoza vipofu. Naye alikuwa na mwana-kondoo aliyemwongoza kwenye nguzo alipoombea. Akasema, “Kitu pekee kilichosalia nilicho nacho, Yehova, ni huyu mwana-kondoo.” Kisha kasema, “Kama utamruhusu tu msichana wangu mdogo aishi, ingawa sijapata kumwona, bali yeye ni faraja kubwa wakati ninapopapasa nywele zake kwa mikono yangu.” Kisha kasema, “Yeye ananipenda, nami ninampenda.” Ndipo kasema, “Yehova, kama utamjalia kuishi, nita—nitakupa mwana-kondoo wangu, kama dhabihu.”

¹³⁰ Basi msichana wake akawa mzima. Naye huyu hapa, akishuka kwenda hekaluni na huyo mwana-kondoo. Ndipo kuhani akaja na kusimama juu ya roshani, na kusema, “Bartimayo kipofu, unaenda wapi, asubuhi ya leo?”

¹³¹ Akasema, “Ninaenda hekaluni, kumtoa sadaka mwana-kondoo huyu.”

¹³² “Loo,” akasema, “Bartimayo kipofu, huwezi kufanya hivyo.” Kasema, “Nitakupa fedha, nawe ushuke kwenye vi—vibanda, ukajinunulie mwana-kondoo ukamtoe sadaka.”

¹³³ Akasema, “Kamwe sikumwahidi Mungu mwana-kondoo fulani. Nilimwahidi mwana-kondoo huyu.”

¹³⁴ Akasema, “Lakini, Bartimayo kipofu, huwezi kumtoa huyo mwana-kondoo, kwa kuwa huyo mwana-kondoo ndiye macho yako.”

¹³⁵ Akasema, “Kama nikiitii ahadi yangu kwa Yehova, Yeye atanipa mwana-kondoo kwa ajili ya macho yangu.”

¹³⁶ Yeye alikuwa, asubuhi hii yenye baridi ya Oktoba, Mwana-Kondoo alikuwa ametolewa kwa ajili ya macho ya Bartimayo kipofu. Kasema, “Mleteni hapa.” Akaweka mikono yake juu ya macho yake, na huyo Mwana-Kondoo aliyetolewa wa Mungu akayafumbua macho yake.

¹³⁷ Enyi marafiki, mwajua, mengi zaidi yangeweza kusemwa kwa hadithi hii kuhusu Yeye akienda hadi kusulibishwa, lakini tutalichukua hilo wakati mwingine baadaye. Je! mwajua, Mwana-Kondoo yule yule ametolewa usiku wa leo kwa ajili ya macho yenu, pia? Mwana-Kondoo yeye yule yupo hapa usiku wa leo. Mungu alimtoa. Hana mwingine, kamwe hatakuwa na mwingine. Huyo ni Mwana-Kondoo wa Mungu aliyetolewa. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹³⁸ Niliangalia saa yangu, tayari niko karibu dakika ishirini ifike saa nne, nami nilikuwa nijaribu kumaliza kwenye saa tatu, tutoke saa tatu na nusu, kwenye wakati wa kawaida.

¹³⁹ Lakini hebu tuviinamisha vichwa vyetu kwa muda mfupi tu. Ninataka kila jicho lifumbwe sasa, na vichwa vyenu viimanishwe. Iweni na uchaji kabisa kwa dakika moja.

¹⁴⁰ “Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi,” akalia yule ombaomba, “Unirehemu.” Naye asingetulia. Ha—hana budi... ha—hana budi kuuvutia usikivu Wake. Basi hamwamini usiku huu ya kwamba kilio chetu kama hicho kitamleta jukwaani tena? Kilimleta wakati huo. Kwa nini kisimlete tena?

¹⁴¹ Sasa wakati mkiinamisha vichwa vyenu na moyo wenu, ninawatakeni mumlilie, “Yesu!” Msimwite Mwana wa Daudi, kwa maana Yeye si Mwana wa Daudi kwenu. Yeye ni Bwana. “Yesu, Bwana, unirehemu. Yafumbue macho yangu yaliyopofuka. Nimemsikia mhudumu huyu aliye pamoja nasi usiku wa leo, akisema ya kwamba Wewe uliahidi kujidhihirisha Mwenyewe kwa uzao wa Ibrahimu, katika siku za mwisho, jinsi ulivyofanya kwa Ibrahimu na uzao wake wa siku ile. Uliliahidi, ya kwamba Wewe ni Neno.”

¹⁴² “Katika siku chache zilizopita usiku, ni—nimekuwa nikiona mambo yasiyo kawaida. Yeye alisema, katika Yohana Mtakatifu, ninajua, 14:12, ‘Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya.’ Na mwanamke huyo akaligusa vazi Lake, Naye akajua shida yake ilikuwa ni nini, na kwa sababu kuwa—kuwa alitumia kiasi hicho cha imani. Mbona, kuamini ya kwamba Yeye alikuwa, imani Yake katika yale aliyokuwa amefanya, Yeye alitangaza kwamba ameponywa, kasema, ‘Imani yako imekuokoa.’ Na kipofu kwenye lango la Yeriko, jambo lile lile. Mtu mtini, asubuhi ya leo, alisamehewa dhambi zake.

¹⁴³ “Yafumbue macho yangu mapofu, Mwana-Kondoo. Nipate kutambua ya kwamba niko katika Uwepo Wake. Ya kwamba Yeye yupo hapa. Wewe ulisema, ‘Walipo wawili au watatu wamekusanyika katika Jina Langu, Ni—Niko miongoni mwao.’ Yafumbue macho yangu yaliyopofushwa, na unirehemu, Ee Mwana-Kondoo wa Mungu.”

¹⁴⁴ Na wakati ukiomba jambo hilo, kama tu kuna shaka lolote niani mwako, kumekuwako na shaka lolote mahali popote kwenye... Sasa tuko tu kwenye mkesha wa ibada kubwa ya uponyaji. Kama kumekuwako na tashwishi yoyote juu yake, hivi huwezi kumwomba ayaondoe magamba yote kutoka machoni mwako, upate kufahamu vizuri?

¹⁴⁵ Siku hizi chache usiku ambazo nimekuwa nikijaribu, kwa moyo wangu wote, kuwafanya mwone jambo fulani, kwamba Yeye anatoa ishara Yake ya mwisho kwa kanisa, kabla hajawageukia Wayahudi. Bibi-arusi wa Mataifa ataitwa.

¹⁴⁶ [Mtu fulani ananena kwa lugha nyingine, halafu anatoa tafsiri—Mh.] Amina. Sasa kama ninaelewa vizuri, wakati mkiomba, Roho Mtakatifu akinena halafu anatoa tafsiri yake, Mungu akiwapa mwaliko.

¹⁴⁷ Ni wangapi hapa ndani wangetaka Mwana-Kondoo wa Mungu aliyetolewa ayafumbue macho yenu, ili mweze kumwona Yeye hapa sasa, akiwapo? Waweza kuinua mkono wako, useme, “Mungu, yafumbue macho yangu mapofu. Jalia utaji wangu uondolewe moyoni mwangu, Bwana, ili nipate kufahamu.”

¹⁴⁸ Na sasa Yeye atajulikanaje? Tutamjuaje? Kwa tabia Yake, kile afanyacho, kazi Zake. Yeye alisema, “Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi.” Sasa, tawi huzaa tunda, sio mzabibu. Mzabibu hulitia tawi nguvu. Na kama tawi likipata kuzaa, ama mzabibu ukizaa tawi, lina zabibu juu yake; mzabibu mwingine ukichipuka, ama tawi kutoka kwenye mzabibu huo, litakuwa na zabibu juu yake. Kama lile kanisa la kwanza lililotoka kwenye mzabibu huo, lilikuwa ni kanisa la kipentekoste, pamoja na karama zote, kama huo kweli ukiwahi kutoa tawi lingine, hao wataandika Kitabu kingine cha Matendo nyuma yake. Na hayo ndiyo waliyokuwa nayo katika siku za mitume, na wakati wa mitume haukuisha kamwe.

¹⁴⁹ Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Na mradi tu Mungu angali anaita, wakati wa mitume ungali unaendelea. “Kwa kuwa ahadi hii,” ahadi kama ilivyokuwa wakati huo, “ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, hao walio mbali, wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

¹⁵⁰ Bwana, yafumbue macho yetu, na utujalie kumwona yule Mwana-Kondoo aliyetolewa. Uliahidi ya kwamba ninii... ya kwamba ungejifunua katika siku za mwisho, kama ulivyofanya Sodoma, wakati Mwana wa Adamu alipokuwa akifunuliwa. Tunaomba, Mungu, ya kwamba utajalia hilo sasa. Sisi ni raia Wako, Bwana. Sisi ni mizabibu Yako.

¹⁵¹ Sisi hatustahili, hatustahili kuomba lolote; bali kama tungewaza juu ya jambo hilo, basi tungekuwa wadogo sana, tungekuwa wasio na faida yoyote. Lakini, Bwana, wakati ninapotazama juu Kule na kuona kuna Mwana-Kondoo aliyetolewa kwa ajili yangu, kuna Mwana-Kondoo aliyetolewa, basi Mungu hanioni mimi, Yeye anamwona Mwana-Kondoo wangu. Nami ninajua Mwana-Kondoo huyo hana dosari yoyote. Amepokelewa tayari.

¹⁵² Sasa, Bwana, jalia Neno la Mungu lijidhihirishe Lenyewe miongoni mwetu, usiku wa leo, kusudi imani ya Bartimayo huyu aliye hapa ndani, kila mmoja wao, na wanawake wanaotokwa na damu na chochote kile, na akina Simoni Petro, na watu mbalimbali walio humu ndani, walio wahitaji, akina Zakayo mtini. Jidhihirishe Mwenyewe, Bwana, kupitia mwili wa mwanadamu. Jalia Neno Lako liwe hai miongoni mwetu, usiku wa leo, tupate kujua na kuona ya kwamba Wewe ni Mungu. Na jalia kila jicho lililopofuka lifumbuliwe lipate kuelewa, Bwana, ili kwamba ibada hii kuu ya uponyaji itakapoanza, jalia kila mmoja wao aponywe. Hawa watoto wadogo wote, na—na watu walio na mikongojo, na—na kasoro yoyote waliyo nayo, wenye fimbo nyeupe, jalia wapate kutembea kutoka hapa kama Bartimayo kipofu alivyofanya. Yeye alifumbuliwa macho. Tujalie, Baba. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

¹⁵³ Sasa tumeomba. Na sasa—sasa kwa uchaji sasa, kwa utulivu, aminini. Sasa kile mimi... Huu mchezo mdogo wa kuigiza, kile ulicho, ama ni kweli au si kweli. Na Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa mngemjua?

¹⁵⁴ Vipi kama mtu fulani angetokea hapa sasa amevaa joho, na ndevu na nywele kama vile wanasanaa wanavyomchora, makovu ya misumari mkononi mwake, na damu ikitiririka kutoka usoni

mwake? Huyu asingekuwa ni Yesu. La. Yeye ameketi mkono wa kuume wa Ukuu; wakati atakapokuja, kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri. Kwa hiyo . . . lakini ungemjuaje? Mnafiki yeyote anaweza kujitia rangi jinsi hiyo na kutenda jinsi hiyo. Hakika.

¹⁵⁵ Lakini utamjuaje? Ni Yeye wakati unapoiona tabia Yake, Neno Lake likidhihirishwa na likifanya vile hasa limefanya daima, ndipo unajua ya kwamba ni Yeye. Hiyo ni kweli? “Kazi nifanyazo Mimi.”

¹⁵⁶ Sasa, unaona, hebu wewe mwenyewe umwamini sasa. Njoo. Usiache akili yako ilale, kama vile watu wasemavyo. Usifanye hivyo. Humjii Mungu, vivi hivi. Unamjia Yeye, ukiwa na akili nzuri, pamoja na Neno Lake. Unalileta Neno mbele yako, na kusema, “Bwana, uliahidi. Nimekuomba uyafumbue macho yangu. Jalia imani yangu imsimamishe Bwana Yesu, usiku wa leo. Jalia anigeukie, na kuniambia kama vile Yeye. . . yule mwanamke aliyefanya hivyo, miaka mingi iliyopita.” Nawe amini kwa moyo wako wote.

¹⁵⁷ Sasa, umbali ninaoweza kuona, kwenye wasikilizaji, hakuna mtu hata mmoja ninayemwona ambaye ninamjua. Ninyi nyote ni wageni.

¹⁵⁸ Na wakati mwingine mnafikiri ni watu hawa huku mbele ndio tu wanaoupata. La, la. Huko . . . Sijali mahali ulipo, wewe amini tu. Sijali, mahali popote jengoni. Yeye anajua wewe ni nani na mahali ulipo.

¹⁵⁹ Sasa angalieni kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kama imani yako inaweza kumsimamisha, kama ya Bartimayo ilivyofanya. Si lazima uwe ombaomba. Haikubidi kupaza sauti kama yeye alivyofanya. Kelele hazikumsimamisha. Yeye hakuzisikia hizo. Imani ndiyo iliyomsimamisha. “Imani yako!” Yeye hakusema “kelele zako zimekuokoa.” “Imani yako imekuokoa.” Mnaona, “Imani yako imekuokoa.” Vema.

Bwana abarikiwe!

¹⁶⁰ Sijui kama yule mhudumu anayeketi pale, yule ndugu mzee ambaye amekuwa akihubiri kwa muda wa miaka sitini na mitano, angenipa fadhila? Utafanya hivyo, bwana? Weka mkono wako juu ya mwanamke huyo anayeketi karibu nawe, nao ugonjwa wa moyo utamwacha. Vema, hivyo tu. Unaamini hilo, dada? Vema, hivyo tu.

¹⁶¹ Yeye aligusa nini? Sijapata kumwona, bali lilitendeka. “Kama unaweza kuamini!” Mnaamini sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁶² Je! hilo linamtambulisha? Macho yenu yamefumbuliwa? Basi hebu mtazameni, Yeye ni wa ajabu, mshindi mkuu! Hakuna kitu, hakuna kanuni za imani, hakuna dhehebu, hakuna mwanasayansi, wala chochote kile, kinachoweza kumzuia. Yeye

ni Mungu. Amina. Ninampa changamoto mtu yeyote hapa aamini hilo, ya kwamba Yeye yupo sasa.

¹⁶³ Ni wangapi waliopata kuiona ile picha ya Malaika wa Bwana kwenye gazeti, waliyo nayo huko Washington? Yeye amesimama papa hapa kwenye jukwaa hili sasa hivi. Kweli! Ninajua Yupo hapa. Ninajua. Mimi si mlokole. Niko mbali na huo. Ninawaambia Ukweli wa Maandiko. Aminini mwone litakalotukia.

¹⁶⁴ Hapa, Huyu hapa tena. Huyu maskini mama mweusi anayeketi hapo mwisho, akiangalia huku na huku. Kweli, anataka fadhila kutoka kwa Mungu. Yeye ni mhudumu, naye anamwomba Mungu amsaidie katika huduma yake. Hiyo si ni kweli, mama? Inua mkono wako, kama hiyo ni kweli. Sijapata kumwona, yeye ni mgeni tu kwangu kadiri maskini yule mwanamke mweusi alivyokuwa huko chini Tennessee wakati ule.

¹⁶⁵ Kuna mtu, mtu mweusi anayeketi pale akikuangalia, kidogo amefurahishwa nayo kupita kiasi. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu, bwana? Unaamini? Yule mwanamke alikugusa kama vile tu wao walivyofanya, kasema, "Jipe moyo." Si mimi ninayekuita, bali ni Yeye anayekuita. Ukiamini hilo kwa moyo wako wote, hicho kisukari kitakuacha. Unaamini hilo? Amina. Vema, basi unaweza kuupokea. Amina. Bwana asifiwe! Jambo ndilo hilo.

Yeye aligusa kitu gani? Kamwe hakunigusa. Alimgusa Yeye.

¹⁶⁶ Hapa, huyu hapa mvulana mdogo, mzungu, ameketi hapa akiniangalia. Shauku kubwa moyoni mwake. Kamwe sikukujua, bali unautafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kweli, wewe. Unaamini hilo? Amini, utaupokea. Unaamini hilo, ewe kijana? Vema, unaweza kuupokea kama utaamini.

¹⁶⁷ Huyu hapa maskini mwanamke mdogo huku nyuma kabisa. Yeye anaugua. Ni mkono wake wa kushoto. Umevunjika. Una kifundo, mkono wa kushoto. Katika mkono wake wa kuume, ana uvimbe wa neva na baridi yabisi. Ataukosa. Bibi Council, unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini ya kwamba Mungu atafanya. . . Umeponywa. Yesu Kristo anakufanya mzima.

¹⁶⁸ Sijapata kumwona mwanamke huyo wala kusikia habari zake, maishani mwangu. Yehova anajua ya kwamba hiyo ni kweli. Amina.

¹⁶⁹ Huyu hapa maskini mwanamke mdogo mweusi ameketi hapa. Anaugua matatizo, mambo mengi. Jambo moja, una shida ya macho yako. Sio kwa sababu umevaa miwani; bali macho yako yanaharibika, kwa vyovyote vile. Una yabisi kavu. Iwapo hiyo ni kweli, pungu mkono wako. Una maumivu kifuani mwako. Hiyo ni kweli? Punga mkono wako. Una ugonjwa wa tumbo. Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako. Unaamini ya kwamba Yeye atakuponya? Unaamini Mungu anaweza

kuniambia kwamba wewe ni nani? Edna Gerald. Kama unaamini kwa moyo wako wote, liamini, nawe unaweza kupokea uponyaji wako. Amina.

¹⁷⁰ Mnaamini Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

¹⁷¹ Vipi kuhusu mwanamke huyu anayeketi hapa mwisho, safu ya pili hapa, akiniangalia moja kwa moja? Ana ugonjwa wa miguu yake. Unaamini ya kwamba Mungu ataiponya miguu yako? Kama unaamini, inua mkono wako. Simjui, sijapata kumwona.

¹⁷² Vipi kuhusu mama anayeketi karibu naye? Unaninii... Angalia upande huu, dada. Unaamini kwamba mimi ni mtumishi wa Mungu, kwa moyo wako wote? Una uvimbe wa neva ambao unakusumbua. Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako. Sasa unaweza kuponywa.

¹⁷³ Mama anayeketi karibu naye, unaamini hilo, kwa moyo wako wote? Unaugua, pia. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Ugonjwa wa figo. Ikiwa hiyo ni kweli, pungu mkono wako.

¹⁷⁴ Mama anayeketi karibu naye, unaamini? Una ugonjwa wa wasiwasi, na wa macho yako. Ikiwa hiyo ni kweli, pungu mkono wako.

¹⁷⁵ Mama anayeketi karibu naye, unaamini, dada? Umetiwa uvuli. Una ugonjwa wa tumbo, ni kansa tumboni. Unaamini Mungu alikuponya? Amina.

¹⁷⁶ Mnaamini? Macho yenu yanaweza kufunguka na kuamini ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu? Basi, ikiwa mnaamini, simameni kwa miguu yenu na kumkubali Yeye, na kuamini kwa moyo wenu wote, ya kwamba ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. "Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!"

Usinipite, Ee Mwokozi mpole,
Kisikie kilio changu kinyenyekevu;
Unapowaita wengine,
Usinipite.

Wewe ni Kijito cha faraja yangu yote,
U zaidi ya maisha kwangu,
Nina nani duniani mbali na Wewe?
Ama ni nani Mbinguni ila Wewe?

¹⁷⁷ Ni jambo gani lililotukia? Imani yako, kama tu yule ombaomba kipofu, imemwita jukwaani. Amina. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, hakuna haja ya mstari wa maombi. Ni wangapi wanaoamini mmeponywa, kwa vyovyote vile? Inua mkono wako, msifu! Amina. Mmeponywa.

¹⁷⁸ Yesu Kristo yuko miongoni mwetu, yeye yule aliyepitia Yeriko, aliyelijua jina la Zakayo, aliyemjua Bartimayo. Bwana

Yesu yeye yule, katika umbo la Roho Mtakatifu, yupo hapa, usiku wa leo, akifanya mambo yale yale aliyofanya, akithibitisha bila kukosea ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Msiruhusu kanuni za imani, na theolojia, na vipindi vya baridi, viwakabe koo. Mko katika Uwepo wa Yesu Kristo, ambaye amedhihirishwa miongoni mwenu. Amina. Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote. Amina.

¹⁷⁹ Ukubali uponyaji wako, useme, “Bwana asifiwe! Ninaukubali.”

¹⁸⁰ Hebu na tuimbe sifa Zake basi. “Nampenda, nampenda.” Je! mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Kwani alinipenda kwanza.” Mnampenda?

Nampenda,

¹⁸¹ Mwabuduni sasa katika Uwepo Wake. Mnajua hana budi kuwa hapa.

...mpenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu

¹⁸² Huo ni uponyaji, pia. Huo ni sehemu ya wokovu wako. Unafanya hivyo wapi? Pale Kalvari—Mtini Kalvari. Mioyo yetu yote!

Nampenda, nampenda,

Limaanisheni kweli. Mwabuduni!

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹⁸³ Loo, hivi hamumpendi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Peaneni mikono na mtu fulani, mkisema, “Bwana asifiwe!” Mkipendana, mnampenda Yeye. Geuka tu na upeane mikono na mtu fulani, ukisema, “Bwana asifiwe! Bwana asifiwe! Tuna furaha kuwa hapa, ndugu, tuna furaha kwamba tuko katika Uwepo wa Bwana Yesu.” Amina. Amina. Ajabu! Loo!

¹⁸⁴ Paulo alisema, “Nikiimba, ninaimba katika Roho.” Na tuabudu katika Roho, tena. Hebu tuimbe katika Roho.

Nampenda, nampenda, (haleluya)
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹⁸⁵ Loo, hivi hamumpendi? Yeye si ni wa ajabu? Imbeni!

Loo wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu,
Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu
Mwenye Nguvu;

Loo huniokoa, hunilinda na dhambi zote na
aibu,

Wa ajabu ni Mkombozi wangu, Jina Lake
lisifiwe!

Loo wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu,
Ndiye Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni
Mungu Mwenye Nguvu;

Huniokoa, loo, hunilinda na dhambi zote na
aibu,

Loo wa ajabu ni Mkombozi wangu, Jina Lake
lisifiwe!

¹⁸⁶ Ni jambo gani lingetukia sasa hivi katika Uwepo wa Mungu,
jinsi hii?

Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, sasa
nimepatikana, nikiwa sina hukumu,
Yesu hutoa uhuru na wokovu kamili;
Huniokoa, hunilinda na dhambi zote na aibu,
Loo wa ajabu ni Mkombozi wangu, Jina Lake
lisifiwe!

Loo, na tuuimbe kana kwamba tunalimaanisha!

Wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu,
Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu
Mwenye Nguvu;

Loo huniokoa, hunilinda, loo, na dhambi zote
na aibu,

Loo wa ajabu ni Mkombozi wangu, Jina Lake
lisifiwe!

¹⁸⁷ Loo, hivi halikufanyii tu jambo fulani, kukusugua kabisa,
upande wa ndani? [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Ushirika, loo,
ni hisia ya jinsi gani! Nisingeweza kubadilisha hili kwa fedha
zote ungaliweza kukusanya, chochote kile. Zitupilie mbali, bali
unipe Yesu. Loo, jamani! Naam, bwana. Ushirika!

¹⁸⁸ Loo, ni tamu jinsi gani kutembea katika njia hii ya
wasafiri, tukiegemea kwenye Mkono wa milele, tukijua ya
kwamba Huyu hapa! Loo, upendo kwa kuonana kwa mara ya
kwanza, kitu fulani ndani yetu kinachoita! Loo, kitu kama
ninii—ninii... kifuniko kilichoondolewa kwenye kisima cha
chemchemi, kikibubujisha tu maji; na kadiri yanavyobubujika,
ndivyo yanavyokuwa baridi na matamu. Amina. Loo, Yeye
ni wa ajabu! Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]
Ninampenda. Nanyi je? ["Amina."] Loo, jamani!

¹⁸⁹ Hivi hampendani ninyi kwa ninyi? [Kusanyiko linasema,
"Amina."—Mh.] Sasa ninyi nyote Wamethodisti peaneni mikono
na Wapentekoste, nanyi Wabaptisti, na muwe na urafiki sana.

Kama hamwezi kufanya hivyo, hamumpendi. Hiyo ni kweli. Maana, wao wanampenda, mnampenda; Yeye alikuchukua wewe na njia zako za kipekee, alifanya hivyo kwa yule mwingine, kwa hiyo hebu tukubali tu sasa. Loo, hivi yeye si ni wa ajabu? [“Amina.”] Tunaamini hilo kwa mioyo yetu yote.

¹⁹⁰ Loo, na tuuimbe tena, wimbo huu mzuri wa kale wa kanisa, “Nampenda, nampenda.”

¹⁹¹ Kamwe siwezi kupata ya kutosha kusema hilo, kwa maana Yeye alinipenda kwanza. Yeye alinipenda mimi, maskini mwana wa mlevi, mwenye mashaka, aliyepofushwa maksudi, anayependa dhambi, nikiwa kwenye ufukara, Naye aliinama chini kwa neema Yake. Sikuwa na uhusiano wowote na jambo hilo. Yeye alinichagua. Naam. Inawezekanaje? Gugu linawezaje kubadilishwa likawa ngano? Inahitaji nguvu za Mungu. Amina. Nampenda. Loo, kidogo na—najisikia kubarikiwa sasa hivi, mimi mwenyewe. Na—na—najisikia vizuri.

¹⁹² Ninajua Yeye yupo hapa. Ni Yeye. Aliahidi hilo. Yeye, Yeye yupo hapa miongoni mwetu. Jinsi ninavyompenda! Yeye ni wa ajabu. Inakufanya ujisikie vizuri kujua ya kwamba haitubidi kubahatisha juu yake. Huyu hapa, akijitambulisha Mwenyewe moja kwa moja katika Neno, kama vile amefanya daima, likimfanya kuwa ni Yeye; sio kanuni fulani za imani, si kitu fulani cha kubuni; bali Mungu aliye hai Mwenyewe. Yeye alijitambulishaje? Si huko chini Sodoma, bali kwa Ibrahimu; na sasa kwa Uzao wa Ibrahimu, baada Yake, inaonyesha sisi ni Uzao wa Ibrahimu. Amina. Loo, jamani! Ninajisikia vizuri sana, sasa hivi.

Nampenda, (Loo, ni manyunyu ya baraka ya
jinsi gani!) Nampenda,
Kwani a- . . .

Hebu wazia tu; kabla hujampenda, Yeye alikupenda!

¹⁹³ Bwana Yesu, jalia uponyaji wa watu hawa, Baba, wapate kuponywa, kila mmoja wao. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba, Bwana, kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

Mtini Kalvari.

¹⁹⁴ Loo, na tuviinamishe vichwa vyetu sasa, kwa utamu, kwa utulivu. Mwajua, sisi ni watoto tu, kwa vyovyote vile. Sisi ni watoto wa Mungu. Ulipata kuona jinsi mtoto alivyo huru akiwa karibu na mzazi wake? Mzazi wake anamwangalia, mnaona. Hebu na tuuvumishe. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.]

¹⁹⁵ Kumwona tu amesimama hapa, Nguzo kuu ya Moto! Yeye alisema, “Nimetoka kwa Mungu; narudi kwa Mungu.” Yeye alikuwa ile Logos iliyokuwa pamoja na Musa nyikani, Nguzo ya Moto. Yeye alikufa pale Kalvari, akafufuka tena. Na wakati

Sauli alipokuwa akienda zake Dameski, Nguzo iyo hiyo ya Moto ilimwangusha chini; akasema, “U nani Wewe, Bwana?”

Akasema, “Mimi ni Yesu.”

¹⁹⁶ Alitoka kwa Mungu; akarudi kwa Mungu. Ametambulishwa kwetu kwa thibitisho la kisayansi, kwa thibitisho la kanisa, kwa kila kitu. “Na. . .” Akileta kitu kile kile Chake, akilitangaza Neno Lake. Yeye Ndiye mfasiri. [Ndugu Branham anavumisha *Nampenda*—Mh.]

¹⁹⁷ Si ingekuwa ni wakati wa kupendeza sana Kwake kuja sasa hivi, aangalie huku na huku na kumwona kila mtu akibadilishwa, akiondoka? Atakuja siku moja. [Ndugu Branham anavumisha *Nampenda*—Mh.]

¹⁹⁸ Sasa tukiwa tumeviinamisha vichwa vyetu, polepole sana. [Ndugu Branham anavumisha *Nampenda*—Mh.]

¹⁹⁹ Kumbukeni, ibada asubuhi. Endapo wewe ni mgeni hapa, na huna kanisa; hawa wachungaji wazuri, wanaiamini Injili ii hii la siyvyo wasingenialika hapa. Wamekaribishwa kwenda kanisani mwao. Mwe na ibada nzuri kesho, usingizi mwema usiku wa leo, kisha mrudi kesho alasiri kwa ajili ya ibada ya uponyaji.

²⁰⁰ [Ndugu Branham anavumisha *Nampenda*—Mh.] Vema. Mungu akubariki, ndugu. 

MUNGU ANAYE MWANA-KONDOO ALIYETOLEWA SWA64-0620E

(God Has A Provided Lamb)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 20 Juni, 1964, katika Ukumbi wa Manispaa huko Topeka, Kansas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org